

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



**HOTUBA YA MH.MKUU WA MKOA KWENYE MAADHIMISHO**  
**YA SIKU YA FAMILIA DUNIANI**

**TAREHE 15.05.2020**

## **1. Historia ya Maadhimisho ya Siku ya Familia Duniani**

Tarehe 15 Mei, ya kila mwaka ni Siku ya Familia Duniani. Siku hii huadhimishwa na Nchi wanawachama wa Umoja wa Mataifa kwa mujibu wa tamko Na.47/237 la tarehe 20 Septemba, 1993. Lengo la maadhimisho hayo ni kutambua umuhimu wa familia na kwamba maendeleo yoyote katika jamii huanzia kwenye ngazi ya familia. Tanzania huungana na Nchi zingine Duniani kote Kuadhimisha Siku hii ya Familia.

## **2. Kauli mbiu ya Siku ya Familia Duniani**

Kaulimbiu ya Siku ya Familia Duniani kwa mwaka 2020 inasema **"FAMILIA NI MSINGI KATIKA KUTOKOMEZA CORONA: TUILINDE NA TUWALINDE WENGINE"**. Kauli mbiu hii inakumbusha na kuisitiza familia kujilinda na mlipuko wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (COVID-19).

## **3. Tahadhali za maadhimisho ya mwaka 2020**

Kutokana na mlipuko wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corana (COVID-19); maadhimisho haya kwa mwaka huu hayafanyiki kwa mtindo wa kawaida wa kuwa na mikusanyiko ya watu. Hivyo, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe inashirikiana na wadau mbalimbali kutoa elimu kwa familia kwa njia zifuatazo:-

- i. Kuimarisha kamati za uhamasishaji jamii kujikinga na COVID-19 katika Halmashauri zote 6 Mkoa wa Njombe.
- ii. Kugawa vipeperushi vilivyoandaliwa na Wizara kwa lengo kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa korona katika Halmashauri zote 6 za Mkoa.
- iii. Kuandaa na kurusha vipindi maalum vyenye kutoa elimu kwa familia na jamii kwa kutumia redio za Kijamii zilizopo mkoani kuhusu wajibu wa familia katika kujikinga na ugonjwa wa Corona.

- iv. Kuwasisitiza viongozi wa kidini kuzingatia na kuwaelimisha waumini wao njia za kujikinga na COVID-19
- v. Kuelimisha jamii kuhusu kujikinga na ugonjwa wa Corona katika halmashauri zote 6 kwenye Mkoa.
- vi. Kuendelea kuisitiza wazazi/walezi kuwalinda watoto kujilinda na maambukizi ya COVID-19 kwa kutozurura mitaani, kuvaa barakoa, kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka mara kwa mara pamoja na kujiepusha na mikusanyiko.

#### **4. Mambo ya kuzingatia katika kujikinga na COVID-19**

Napenda kutumia maadhimisho haya, kuwasisitiza wananchi wote wa Mkoa wa Njombe kuzingatia mambo yafuatayo ili kujikinga na ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (COVID-19):-

- i. Kunawa mikono kwa kutumia maji safi tiririka na sabuni au kutumia vitakasa mikono.
- ii. Kujiepushe na mikusanyiko na safari zisizo za lazima, kuvaa barakoa kila inapobidi
- iii. kujiepushe kupeana mikono na kukumbatiana
- iv. Unapopiga chafya au kukohoa ziba mdomo na pua kwa sehemu ya ndani ya kiwiko cha mkono
- v. Kula chakula bora mfano kuku, samaki, nyama, maziwa, mayai, matunda na mboga mboga ili kuimarisha kinga ya mwili na
- vi. Fanya mazoezi ya viungo mara kwa mara.
- vii. Wazazi na walezi, hakikisheni watoto wanabaki nyumbani, waandaliwe michezo ya kuwaburudisha na watoto wa shule waendeleo kujisomea.

Kwa taarifa na msaada kuhusu ugonjwa wa CORONA; piga simu ya bure namba 199.

Nawakumbusha kwamba ugonjwa wa Corona upo na bado ni tishio katika maisha yetu, hivyo tusipuuzie tahadhali zinazotolewa na Wataalam wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**“NJOMBE BILA CORONA INAWEZEKANA: TIMIZA WAJIBU WAKO  
KWA KUZINGATIA USHAURI WA WATAALAM WA AFYA”**

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**

**MUNGU IBARIKI NJOMBE**

**ASANTE KWA KUNISIKILIZA**